## TARATIBU ZA KUFUATA BAADA YA KUPATA KIBALI CHA UJENZI

Kwa niaba ya sheria ya ujenzi mijini ujenzi wowote ambao umepata kibali unapaswa kukaguliwa kwa kila hatua ya ujenzi.

**Baada ya kupata kibali cha ujenzi yanapaswa kufanyika**

1. Kutoa notisi ya masaa 48 kabla ya kuanza ujenzi. Fomu ya notisi utapatiwa unapokabidhiwa kibali cha ujenzi

2. Kujaza fomu ya ukaguzi na kuwasilisha kwenye ofisi ya ujenzi unayotaka kufanya ikaguliwe.

3. Utapatiwa "Certificate of Occupation" baada ya ujenzi wako kukamilika iwapo tu hatua muhimu za ujenzi zimekaguliwa

**NOTE: Kwa sheria ya mazingira ya mwaka 2004 kifungu cha 4 (1) (a), (b) (2) na (3) inasisitizwa kuwa ujenzi wa majengo makubwa kama vile majengo marefu, maghala,viwanda na vituo vya mafuta ni lazima maombi yake yaambatanishwe na RIPOTI YA ATHARI YA MAZINGIRA ( E.I.A ).**

## FAIDA ZA KUJENGA NYUMBA IKIWA NA KIBALI CHA UJENZI

1. Kuishi kwenye nyumba ambayo imethibitishwa kitaalamu kuwa ni salama

2. Kuwa na mazingira bora kwa kuwa na mji uliopangwa

3. Kuepuka hasara na usumbufu unaoweza kutokea iwapo ujenzi umefanyika bila kibali ikiwa pamoja na kushitakiwa mahakamani, kuvunjiwa na kulipa gharama za uvunjaji

**Kwa maelezo zaidi wasiliana**

**Mhandishi wa manispaa**
**Halmashauri ya Manispaa ya Temeke**
**Barabara ya Mandela karibu na**
**Uwanja wa Taifa**
**S.L.P 46343**
**Dar es Salaam**
**Tel: 2841054**
**Email: temekemanispaa@raha.com**

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

TEMEKE MUNICIPAL COUNCIL

BANDARI YA SALAMA

# KIBALI CHA UJENZI

(Building Permit)